**Kila mtu ana malaika (01) - Kuficha ukweli.**

Mwandishi: Romie Singh - Mhariri: Saumu Mwasimba

**Wahusika**

Anita (36)
Angela (17)
Annie (16)
Tom (18)
Djamila (17)
Wasichana na wavulana wenye umri kati ya miaka 15 na 17
Mwalimu wa kiume (40)

**Utangulizi**

Karibu katika kipindi cha Sikiliza ujifunze kipindi kinachohusu mfululizo mpya wa mchezo wa Radio kwa jina "Malaika wa kila mtu".

Katika mfululizo huu wa vipindi kumi vya mchezo wa Radio tutayafuatilia maisha ya vijana wanne wanaosoma katika shule moja. Angela mwenye umri wa miaka 17 amelelewa katika maisha ya nidhamu kali, Annie (16) mama yake sio hata kidogo, Djamila (17) familia yake inamlinda sana na Tom (18) ni kijana anayeonekana anafahamu kitu gani anachokitaka.

Hata hivyo vijana wote hawa wanne wanaweza kudhuriwa kutokana na ushawishi wa makundi ya vijana walio wakubwa kwao wa watu wazima na hata hatari ya kutumbukia katika janga la kuishi na virusi vya HIV na Ukimwi.

Katika kisa cha kwanza cha mfululizo wa mchezo "Malaika wa kila mtu" tunaungana na msichana Angela wakati akikabiliwa na mamake kutokana na kumficha ukweli juu ya hali yake. Lakini je kweli Angela alikuwa akiijua hali yake? Karibu.

**SURA 1: Sebuleni**

*Sauti za asubuhi.*

ANITA: (Akiwa na taharuki) Unawezaje----unawezaje kunifanyia hivi wewe… (akitokwa na machozi) nilikutaja jina la Angela mwanangu baada ya kudhania kuwa ulikuwa malaika. Lakini sivyo, sio malaika wewe! Malaika hawawaangushi mama zao namna hii. Aah mwananguuu….

Angela: ( Akilia) Mama nisamehe mama. Sikujua nisamehe tafadhali mama naomba msamaha.

ANITA: Ni kwa muda gani umeyajua haya?

ANGELA: Sijui, sikujua ma-ma si…
ANITA: Usinambie upuuzi huo umesikia…

ANGELA: Sivyo ma! Sikujua, nilidhani ni mchezo tu kwamba siku zangu za mwezi haziji lakini nilikua na woga wa kukuuliza mama.

ANITA: Na hilo tumbo lako enhe - namaanisha kwa nini sikuoni unapovua nguo. Lakini unaona - kwani huoni wakati ukioga kwamba tumbo lako linavimba?

ANGELA: Ndio nimeona lakini nilifikiri kwamba ni jambo la kawaida tu mama, wewe ndio mamangu na hukutambua!

ANITA: Alaaaa, sasa mimi ndio nimekuwa wa kulaumiwa sivyo! Sasa naona umevuka, umevuka mpaka, nimefanya bidii zote kukulainisha na kukufanya ufuate mkondo mwema…

ANGELA: Ndio mama..

ANITA: Sasa kwa nini niliyafanya yote hayoo, kwa nini nilipata tabu hiyo enhe, nikaweka sheria, na nidhamu zifuatwe, ikiwa ulipata fursa ya kwanza - au labda hata haikuwa mara ya kwanza? Pengine ushayafanya mambo haya hapo kabla… (akipaza sauti tena kwa ukali) Pengine wewe ni hawa hawa wa mitaani Ahhh mwanangu! (Alia kwa uchungu)

ANGELA: Tafadhali mama si hivyoo… nisamehe mama pole mama haikuwa kusudio langu.

ANITA: Haya basi la shule linakuja, sitaki hata kuendelea kuzungumza na wewe. Nenda, nenda zako!

**SURA 2: Ndani ya basi wakielekea shule**

*Kelele za kuimba, wakipigana na kucheza wasichana na wavulana wenye umri wa miaka 15+.*

TOM: Vipi Annie, nimefurahi sana kukuona ndani ya basi la shule - angalau ni mabadiliko.

**Kila mtu ana malaika (01) - Kuficha ukweli.**

Mwandishi: Romie Singh - Mhariri: Saumu Mwasimba

ANNIE: Una maana gani?

TOM : Liko wapi gari la kuvutia ambalo kila siku unakuja nalo?

ANNIE: Tafadhali Tom fuata yanayokuhusu.

TOM: (Kwa njia ya kimapenzi) Kwani umebadilisha wazo la kukutana na mimi baada ya shule?

ANNIE: Well, utafanya nini kubadili fikra zangu Tom? Mpaka sasa sijaona hata chembe ya sababu moja nzuri kutoka kwako ya kwa nini nimdanganye mamangu kwamba tuna mazoezi ya michezo? Kitu gani kitanifanya nifanye hayo enhee?

TOM: Niko kwa ajili yako Gal! Hiyo ndo sababu eti!

ANNIE: Samahani Tom hiyo sio sababu ya kutosha umesikia! Kuna wengine wengi ambao wanavyo vyakutoa na isitoshe wanavutia! (kwa madaha)

TOM : Oh - unamaanisha kama - kama vile magari ya kifahari ?

DJAMILA: (Off Mic) Nyie wawili nini kinachowahamakisha hapo ehe? Tom? Unamsumbua dadangu?

Tom: (Turned off) La la sio hivyo Djamila - na wala hayakuhusu. Lakini Annie una hakika una fikra za ajabu kuhusu kutongozana. Argh! achana nayo twendelee na sahau kama hata nilikuuliza jambo hilo.

*SAUTI ZA WAVULANA WAKICHOKOZANA.*

BOY 1: (Off Mic) Annie ameishiwa huyo, anafuata wanaume wenye fedha tu! Au sivyo Annie?

ANNIE: Funga domo lako wewe kono kono mdogo. Ingie ndani ya gamba lako.

*Wasichana wajiunga, wakiita majina ya wanaume*

ANGELA: Ah acheni bwana nyie, siwezi kusikiliza kelele zenu bwana nyamazeni.

**Kila mtu ana malaika (01) - Kuficha ukweli.**

Mwandishi: Romie Singh - Mhariri: Saumu Mwasimba

DJAMILA: Ah vipi swahiba?

ANGELA: Kichwa kinaniuma, hebu tafadhali niache kama nilivyo.

DJAMILA: Sawa rafiki nakuacha, lakini kijana anayetesa yule ni kijana anayetesa hapa shule? na unamuweka paki namna ile? Annie eti unasemaje?

ANNIE: Nimemwambia vile ilivyo, sina haja ya kwenda na yeye ikiwa hilo tu ndo analolihitaji. Jake atanipa lift ya kwenda shule, kijana mzuri anayevutia kimaumbile ennhe tena aliwahi hata kunitunukia simu hii ya mkononi. Angalia!

*Simu ya mkono: Mlio mpya wa simu*

DJAMILA: Wow tazama kitu cha nguvu, angalia Angela!

ANGELA: Naam ni kitu kweli.

DJAMILA: Oh! Samahani, (anamgeukia Annie) sasa kuna mpango gani?

ANNIE: Sasa hilo inabidi umwambie swahiba yangu hapa Djamila. (Wote Wakichekacheka) Lakini kitu ambacho sihitaji ni mama yangu kugundua. Kwa hivyo dada itabidi uyanyamazie sawa? Wewe pia Angela umesikia.

ANGELA: Kwa kweli mamangu hata hashughuliki kunizungumzia tena kwa hivyo siri yako imefika ndipo haitoki nje hiyo usitie shaka.

DJAMILA: Hey Annie! Kweli! Sijui unafanya vipi. Mamangu nakwambia ni mkali kweli. Kweli anahitaji kujua kila kitu hata nikichelewa dakika mbili kutoka shule.

ANGELA: Ah mwenzangu huyo ni kama mamangu

DJAMILA: Ila mimi naweza tu kwenda out kubarizi ikiwa kaka yangu atakuwa pamoja nami - vinginevyo haiwezekani mwenzangu.

ANNIE: Ah nyie waislamu wajua mna nidhamu kweli, lakini sisi - ahh kwa mfano bibi yangu: Anaweza kuwa mkali ikiwa anaishi na sisi. Mama yangu wala hashughuliki yuko laini tu na wala mimi sijawahi kumjua baba yangu. Na ikiwa mjomba wangu

ataonyesha kujishughulisha shughulisha mara kwa mara huwa kuna sababu fulani mbaya.

ANGELA: Mie mjomba wangu ni mzuri kweli lakini mamangu lo hafikirii hivyo.

DJAMILA: Annie wasema nini - anavutiwa na mambo yasiyokuwa mazuri?

ANNIE: Ah bwana wee Djamila! Wajua nnachokimaanisha. Kwa wewe huna mjomba ambaye huwa karibu sana na wewe mara nyingine? Wacha zako, huwezi kunambia kwamba nyote nyie kwenu ni malaika ah wacha?

MUSIC BRIDGE

**SURA 3: Darasani mwalimu akifunza biologia**

*Minong'ono na vicheko.*

TEACHER: Njia za uzazi zipo upande wa kushoto na kulia kama ilivyochorwa katika diagramu hii. Yai la uzazi au Ovum linateremka chini katika upande wa kulia wa njia ya uzazi mwezi mmoja na upande wa kushoto wa njia za uzazi katika mwezi unaofuata.

*RECORD FOLLOWING TEXT SEPARATELY: FADE UNDER NEXT DIALOGUE:*

TEACHER: Fungueni ukurasa wa 56 kuna njia mbili za uzazi zilizounganishwa aidha na mojawapo ya mwishoni mwa utumbo na kila moja inaishia karibu na yai la uzazi na kuunda kinachoitwa Fimbria. Njia za uzazi hazishikani moja kwa moja na mayai, lakini zinabaki wazi katika tumbo, kwa maneno mengine ni ndani ya tumbo. Na hapo zinaunda mawasiliano ya moja kwa moja kati ya tumbo na nje ya utupu wa mwanamke.

ANGELA: (Anakoroma kwa sauti ya chini) Ouch…

DJAMILA: Nini tena Angela? Uko sawa?

ANGELA: Hapana nafikiri nitakuwa mgonjwa - tafadhali niache… acha… (retching)

DJAMILA: Mwalimu - mwalimu!

*Mwisho, sauti inafifia.*

TEACHER: Kuna nini, nini Djamila

DJAMILA: Tafadhali mwalimu, Angela anahitaji kutoka nje kidogo, hajisikii uzuri - anaumwa!

*Vurumai darasani.*

TEACHER: Shh! Shh tulieni nasema hebu wekeni njia hapa… hebu njoo Angela.

*Milango ya darasa inafunguka.*

TEACHER: Hebu tulieni, nyamazeni. Djamila! Mchukue Angela uende nae na baadae urudi unipe ripoti baada ya darasa. nyinyi wengine nyamazeni! Silence.

*Darasa kimya.*

TEACHER: Sasa tulikuwa tumefikia wapi? Ok yes, ukurasa wa 56. Ndio. Wakati ovari ikijiunda na kuwa yai kamili la uzazi, linajikusanya katika kifuko - *(FADE OUT)* - maalum cha uzazi. Mayai ya uzazi na kifuko hicho pamoja na ukuta unaozunguka mayai hayo ya uzazi vikishakomaa hutumbuka. (END)

**SURA 4: Sebuleni**

*Sauti ya ufunguo. Mlango unafunguliwa.*

ANITA: (Off Mic. Kwa sauti ya ukali.) Angela?

ANGELA: (akijongea) Naam Mama.

ANITA: (Coldly) Eeeh, baada ya mazungumzo yetu leo asubuhi - ni wazi kwamba umekuwa kimya kuhusu kuzungumzia habari ya wewe kukutana na kijana ye yote. Nilikuamini mwanangu

nilipokuwa nikikuruhusu kwenda kukaa na binamu zako. Sasa unajua kwamba umevunja amri zangu zote na hata zile za Mungu wako.

ANGELA: Ndio mama.

ANITA: Sasa nasema hivi, sitaki kukuona ndani ya nyumba hii. Nnachotaka ukifanye sasa hivi ni uhame ukaishi huko huko kwa huyo mvulana wako alokutunga hiyo mimba!

ANGELA: (Akihema kwa pumzi nzito) Mama hapana - tafadhali mama usinifanyie hivyo, simjui kijana mwenyewe. Anaishi karibu na kwa mjomba ni kilomita 20 kutoka hapa mama mama. Siwezi siwezi (akilia) nataka kuishi hapa na wewe mama!

ANITA: (FIRMLY) Sawa sawa kwanza tuangalie moja. Nataka kujua ukweli, pengine huna hata hiyo mimba? Nafikiri inabidi twende ukapimwe. Nataka ufanyiwe uchunguzi barabara… Nna maana twende kliniki sasa hivi, tena nakupeleka mwenyewe, na kwa taarifa yako tutayasubiri majibu mpaka yatoke hata ikiwa itatubidi tukeshe tukisubiri niko radhi mwanangu, ili mradi tuupate huo ukweli wa mambo. Kisha nitajua cha kukifanya. Tumeelewana?

**Hitimisho**

"Malaika kwa kila mtu" ni mchezo wa redio uliotungwa na Romie Singh. Ni hayo tu kwa leo kutoka makala ya sikiliza ujifunze. Ungana nasi wiki ijayo katika kisa cha pili cha mchezo huo, ambapo Angela anazidi kukataliwa na mamake huku akionewa huruma kidogo na madaktari. Hali kadhalika tega sikio wiki ijayo ung'amue jinsi msichana Annie anavyojihatarisha kutokana na mtindo wake wa maisha.

Kumbuka ukitaka kusikiliza kipindi hiki kwa mara nyingine au una marafiki unataka wasikilize, tembelea tovuti yetu, anuani ni www.dw-world.de/lbe.

Kwa heri.